# Huduma za Nyumbani na za Kijamii za Nebraska Medicaid (HCBS)

## Jeraha la Ubongo (TBI) Waiver

# MWONGOZO WA HARAKA WA HUDUMA

*Mwongozo wa Haraka ni utangulizi wa huduma na inaweza kutumika ili kuamua huduma zipi za kuzingatia. Mratibu wa Huduma ata eleza huduma kwa maelezo zaidi na kujadili chaguzi za mtoa huduma.*

*Huduma hupatikana kulingana na mahitaji yako. Mchanganyiko wa huduma unaweza kuhitajika ili kuzingatia sheria za programu.*

NEBRASKA
Good Life. Great Mission.
DEPT. OF HEALTH AND HUMAN SERVICES

2023

## SIKU YA AFYA KWA

Siku ya Afya kwa Watu wa kubwa wa TBI ni pamoja na shughuli za kijamii na afya zinazo tolewa inje ya nyumba ya mshiriki. Inajumuisha tunzo kibinafsi, tathmini la afya na huduma za uuguzi, huduma za chakula, huduma mpya za usaidizi wa tiba, na shughuli zingine.

## USAIDIZI WA TEKNOLOJIA

Usaidizi wa teknolojia ni pamoja na kununua au kukodisha vitu, vifaa, au mifumo ya bidhaa ili kuongeza au kudumisha uwezo wako wa kufanya shughuli za kawaida za kila siku.

Huduma hii inajumuisha kubuni, kufaa, kurekebisha na kutunza vifaa, pamoja na mafunzo au msaada wa kiufundi wa kutumia vifaa. Huduma hii ni kwa pamoja na tathmini ya tambua aina gani ya usaidizi wa teknolojia unahitaji.

## MAZOEZI YA MWUGUZI

Mafunzo ya Uuguzi hutoa mafunzo na elimu kwa muuguzi wako asiyelipwa ambaye hutoa misaada isiyo rasmi.

## KAZI

Kazi ya kusaidia katika kudumisha afya na usalama ndani ya nyumba yako mwenyewe. Kazi hukua mara chache zaidi kuliko TBI Companion.

Kazi ni kwa pamoja na shughuli za utunzaji wa nyumba kama vile kusafisha nyumbani na kutunza vifaa vya nyumbani, vifaa, au vyombo; matengenezo madogo ya madirisha, skrini, hatua au njia panda, vyombo, na vifaa vya nyumbani; na mandhari. Utunzaji wa mazingira ni kwa pamoja na uondoaji wa theluji na barafu, ukataji, uchakachuaji, kuondoa takataka (kwenye mahali pa kuchukua taka), kuondoa wa wadudu, na kusafisha mifereji ya maji.

## MAHUSIANO NA JAMII

Msaada kwa Ushirikiano wa Jamii hukusaidia kushiriki katika shughuli za jamii.

## MWENZI

TBI Companion ni kwa pamoja uchunguzi na usaidizi wa kijamii unaotolewa nyumbani kwako na huenda kwenye mazingira ya jamii. Huduma hii inaweza kujumuisha kazi nyepesi za utunzaji wa nyumba, kulipa bili, huduma ya dharura, ununuzi muhimu, utayarishaji wa chakula, na huduma ya kufulia.

## MAREKEBISHO YA NYUMBANI

Marekebisho ya nyumba ni mageuzi kwa nyumba yako ili kuongeza au kudumisha uwezo wako wa kufanya shughuli za kawaida za kila siku, hufanya iwe rahisi na salama kuzunguka na kufanya mambo yako mwenyewe. Marekebisho yanaweza kusaidia kufikia nyumba yako vyema na kuhitaji msaada ndogo kutoka kwa watu wengine.

## VYAKULA VINAVYOPELEKWA NYUMBANI

Vyakula vinavyopelekwa nyumbani vinapelekwa nyumbani kwako, kupitia msaada wa vyombo vya usafi, na vifaa, kudumisha halijoto sahihi ya chakula, na vyenye theluthi moja ya mahitaji ya kila siku ya lishe kwa watu wazima, kwa kutumia aina mbalimbali za vyakula siku hadi siku. Unaweza kuwa na ustahiki wa kupata chakula kinacholetwa nyumbani ikiwa huwezi kutayarisha chakula chako mwenyewe.

## USAFIRISHAJI USIO WA MATIBABU

Usafirishaji usio wa matibabu hutoa usafirishaji kwenda na kutoka kwa rasilimali za jamii ili kukusaidia kuendelea kuishi nyumbani kwako.

## KUJITUNZA BINAFSI

Matuzo Kibinafsi TBI ni pamoja na usaidizi wa shughuli za kila siku (ADL) na kazi zinazo husu afya na inaweza kujumuisha shughuli muhimu za maisha ya kila siku (IADL). Inatolewa kwa nyumba yako au jamii.

Huduma hii inakusaidia kumaliza kazi ambayo unafanya binafsi ikiwa haukuwa na TBI.

## MFUMO WA JIBU LA DHARURA KIBINAFSI (PERS)

PERS ni chombo cha kielektroniki kinachotumiwa kukusaidia kuwasiliana na mtu katika dharura. Mfumo unaunganishwa na simu yako na inajulisha mtu aliyeteuliwa au kituo cha simu unapobonyeza kitufe.

## RESPITE

TBI Respite ni huduma ya muda mfupi ambayo unaweza kutumia wakati huwezi kujisaidia. Respite ni utulivu wa muda kwa muuguzi wa kawaida anayeishi nawe. Mtoa huduma wako husaidia kushughulikia maisha yako ya kila siku, matengenezo ya afya na uchunguzi.

## AJIRA INAYOSAIDIWA– UCHUNGUZI

Ajira Inayosaidiwa – Uchunguzi hukusaidia kuweka kazi yako ya ushindani. Huduma hii inaweza tolewa kwako au kwa kuwasiliana na mwajiri wako kwa ajili yako.

## AJIRA INAYOSAIDIWA– MTU BINAFSI

Ajira Inayosaidiwa– Mtu binafsi hutoa mafunzo ya kazi kupitia mafundisho ya moja kwa moja ili kukusaidia kuweka kazi yako ya ushindani. Huduma hii hutolewa kazini kwako. Mtoa huduma wako hukusaidia na ujuzi wa kazi na rufaa kwa ajili ya rasilimali nyingine.

## MAISHA YA MAKAZI YALIYOSAIDIWA

Maisha ya Makazi Yaliyosaidiwa iliitwa hapo awali Kuishi kwa Msaada. Inatoa makazi, chakula na huduma zingine, kama vile usaidizi wa shughuli za matunzo kibinafsi, shughuli za maisha ya kila siku (ADL), shughuli muhimu za maisha ya kila siku (IADL), na kudumisha afya. Maisha ya Makazi Yaliyosaidiwa hutolewa katika kituo cha kusaidiwa kuishi kilicho na leseni kupitia Afya ya Umma na kusimamiwa na Medicaid na Huduma ya Muda Mrefu (MLTC).

Unalipa chumba na bodi na sehemu yoyote ya Medicaid ya gharama inayotumika.

## MAGEUZI YA GARI

Mageuzi ya Gari ni mabadiliko kwa gari ili kukidhi hitaji lako la kujumuika kikamilifu katika jumuiya. Mageuzi yatasaidia kufikia vema gari lako na hitaji la msaada kutoka kwa watu wengine itakuwa ndogo.

*Kwa maelezo zaidi kuhusu huduma hizi, na kuona ni zipi unastahiki, wasiliana na Mratibu wako wa Huduma. Huduma zako zinapaswa kutambuliwa ndani ya mpango wako kabla ya mtoa huduma kupewa ruhusa ya kutoa huduma kwako.*